

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole  
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## **TANGAZO KWA UMMA**

### **MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA NGUDU (NGUDU WSSA) KWA MWAKA 2018/19**

Mnamo tarehe 5 Machi 2019, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi ya marekebisho bei na ada kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngudu. Maombi hayo yametokana na kupanda kwa gharama za maji ya jumla kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA) kwa asilimia 38 na kuanza kutekelezwa 1 Januari 2019. Jedwali hapa chini yanaonesha muhtasari wa maombi hayo.

#### **Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi (Shilingi/Uniti)**

<b>Kundi la Wateja</b>	<b>Bei za Sasa</b>	<b>Mabadiliko kwa asilimia</b>	<b>Bei zinazopendekezwa</b>
	<b>2018/19</b>		<b>2018/19</b>
Majumbani	1,137	32%	1,500
Taasisi	1,275	37%	1,750
Biashara	1,928	35%	2,600
Magati	1,500	33%	2,000
Kuosha na ufundi wa magari	2,274	23%	2,800

**Jedwali 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)**

Kundi la Wateja	Ada za sasa	Mabadiliko kwa asilimia	Ada Zinazopendekezwa
	2018/19		2018/19
Majumbani	5,500	173%	15,000
Taasisi	5,500	264%	20,000
Biashara	5,500	173%	15,000
Kuosha na ufundi wa magari	5,500	173%	15,000

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, EWURA inaanzisha mchakato wa kupata maoni ya wadau ili kujua uhalali wa maombi iliyoyapokea.

Nakala ya maombi na nyaraka za Ngudu zilizowasilishwa EWURA zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi kati ya saa 3 asubuhi na saa 10 jioni katika ofisi za EWURA. Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa ili kufanikisha zoezi hili.

Katika mchakato huo, EWURA itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwamo Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa huduma (CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) pamoja na wananchi. Wadau wanaopenda kutoa maoni yao wataombwa kuwasilisha maombi yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kuyatuma kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonyeshwa hapo juu ndani ya kipindi cha wiki mbili baada ya tangazo hili. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **OFISI ZA EWURA KANDA YA ZIWA, GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF – BARABARA YA KENYATTA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA NGUDU**.

**Imetolewa na:**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

**10 Aprili 2019**

